*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 20 Aprili, 2020

*(Bunge Lilianza Saa Nane Kamili Mchana)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu!

**NDG. RAMADHANI ABDALLAH-KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU:

*(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)*

Na. 103

### Ujenzi wa Ofisi za Watendaji wa Kata

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Kusogeza huduma karibu kwa wananchi ni pamoja na kuweka mazingira bora ya kufanyia kazi lakini katika baadhi ya miji na vijiji Watendaji wa Kata hawana ofisi za kufanyia kazi wala samani za ofisi:-

Je, Serikali ipo tayari sasa kujenga Ofisi za Watendaji wa Kata?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kujenga Ofisi za Watendaji wa Kata nchini kwa awamu ambapo katika mwaka wa fedha 2019/2020, jumla ya shilingi milioni 964 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Kata 46. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 1.67 kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Kata 125 nchini.

Na. 104

**Sera ya Kituo cha Afya kila Kata na Zahanati kila Kijiji**

**MHE. DKT. STEPHEN L.KIRUSWA** aliuliza:-

Sera ya Taifa ya Afya inatamka kwamba, kila kijiji kinastahili kuwa na zahanati, kituo cha afya kila kata na kila wilaya kuwa na hospitali ya wilaya:-

Je, ni lini mkakati wa Serikali kuhakikisha kuwa vijiji 22 vya Wilaya ya Longido ambavyo havina zahanati na Kata ambazo hazina vituo vya afya vinapatiwa huduma hizo muhimu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mhesimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Sera ya kuwa na zahanati kila kijiji, kituo cha afya kila kata na hospitali kila wilaya unafanyika kwa awamu. Hadi Machi 2020, Serikali

imekamilisha ujenzi wa Vituo vya Afya vya Engaranaibo na Longido kwa gharama ya shilingi bilioni 1.1 katika Wilaya ya Longido.

Aidha, Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Longido imejengwa kwa gharama ya shilingi bilioni 1.5. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imepanga kuendelea na ujenzi wa zahanati tatu katika halmashauri 184 ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Longido.

**MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya swali langu kuhusu sera ya ujenzi wa huduma za afya kila kijiji, kata na wilaya na shukrani zangu za dhati kwa Serikali kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Longido kwa miradi iliyotekelezwa, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; je, Serikali imetenga shilingi ngapi katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kuendeleza kazi zilizobakia ili kukamilisha ujenzi wa Vituo vya Afya vya Engarenaibor, Eorendeke na Ketumbeine (ambayo imejengwa kwa nguvu ya wananchi) pamoja na Hospitali ya Wilaya ya Longido?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa wananchi wa vijiji vitatu vifuatavyo wamefanikiwa kujenga hadi ngazi ya maboma zahanati kwa nguvu zao kwa kutambua umuhimu wa kuwa na huduma za afya karibu. Je, Serikali iko tayari kuwasaidia kuzikamilisha zahanati hizo mwaka huu? Zahanati hizo ziko katika Vijiji vya Mundarara, Kitongoji cha Injalai; Kijiji cha Leremeta, Kata ya Sinya; na Kijiji cha Gelai Lumbwa, Kitongoji cha Esokonoi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Stephen L. Kiruswa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2020/2021, imetenga fedha shilingi bilioni 27.75 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati nchi nzima. Kwa upande wa Longido Serikali imetenga shilingi milioni 150 kwa ajili ya kukamilisha maboma matatu katika halmashauri hiyo. Serikali pia imetenga fedha shilingi milioni 500 katika mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ajili ya umaliziaji wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Longido. Pia katika mwaka wa fedha 2020/2021, halmashauri hiyo imetengewa shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu na ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya Hospitali ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele vya maeneo ya ujenzi/ukarabati au ukamilishwaji wa maboma vinawasilishwa na halmashauri husika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuwekwa kwenye mipango ya utekelezaji. Kwa hiyo, tunategemea Halmashauri ya Longido itawasilisha maeneo ya kipaumbele kwa ajili ya ukamilishwaji wa maboma ya vituo vya kutolea huduma za afya vilivyojengwa kwa nguvu za wananchi.

Na. 105

## Kuondoa Ufisadi Nchini

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA** aliuliza:-

Je, ni kweli Serikali ina mkakati wa kuondoa aina zote za ufisadi nchini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Serikali ina nia ya dhati ya kuondoa aina zote za ufisadi nchini. Kwa dhamira hii Serikali imeifanyia marekebisho Sheria ya Uhujumu Uchumi,

Sura ya 200 kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) ya Mwaka 2016 kwa kurekebisha vifungu kadhaa kwa kupanua wigo na kuongeza makosa ya uhujumu uchumi pamoja na kuanzisha Divisheni ya Mahakama ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu (Mahakama ya Ufisadi na Uhujumu Uchumi) katika Muundo wa Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua athari za rushwa kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini Serikali imebuni na kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu *(NACSAP III)* wa Mwaka (2017 – 2022). Mkakati ni shirikishi na unalenga kuzuia na kupambana na rushwa katika sekta za uchumi za kimkakati zenye mazingira shawishi ya rushwa ambazo ni Manunuzi ya Umma, Ukusanyaji wa Mapato, Uvunaji na Matumizi ya Maliasili, Madini, Nishati, Mafuta na Gesi, Utawala, Vyombo vya Utoaji wa Haki na Shughuli za Vyama vya Siasa. Aidha, Serikali imeanzisha Kitengo cha Urejeshaji Mali chini ya TAKUKURU kwa ajili ya urejeshaji mali zilizopatikana kwa njia za rushwa *(Asset Tracing and Recovery Unit).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha Disemba, 2015 hadi Machi 2020, TAKUKURU kupitia Kitengo Maalumu *(Asset Tracing and Recovery Unit),* imefanikiwa kuokoa zaidi ya shilingi bilioni 249.4. Imetaifisha nyumba nane zenye thamani ya shilingi bilioni 11.63; magari matano yenye thamani ya shilingi milioni 126 na viwanja vinne. Serikali pia imefanikiwa kuzuia shilingi bilioni 52.8, *USD* 61.1 milioni; magari 14 yenye thamani ya shilingi 635; na nyumba 15 zenye thamani ya shilingi bilioni 13.95.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imesimika Mfumo wa Ukusanyaji Mapato ya Serikali *(Government Electronic Payment Gateway - GePG*) kwa lengo la kuziba mianya ya uvujaji wa mapato. Aidha, Serikali imeunganisha mifumo mbalimbali ya TEHAMA ili kuboresha utoaji wa huduma na kupunguza urasimu na mianya ya rushwa nchini.

Na. 106

**Serikali Kujenga Ofisi za TAKUKURU – Kyerwa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Wilaya ya Kyerwa ni miongoni mwa wilaya ambazo hazina Ofisi ya TAKUKURU kitu ambacho kimeongeza vitendo vingi vya rushwa na wananchi kutotendewa haki hasa upande wa Mahakama na Polisi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Ofisi za TAKUKURU au kuleta huduma hiyo Wilayani Kyerwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali tayari imefungua Ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Kyerwa tangu mwezi Aprili mwaka 2018 na huduma za ofisi hiyo zilizopo eneo la Rubwela zilianza rasmi tarehe 18 Septemba, 2018 tofauti na awali ambapo huduma hizo zilikuwa zinatolewa huku watumishi wakitokea Wilaya ya Misenyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uhitaji mkubwa wa ujenzi wa majengo katika ofisi mbalimbali za TAKUKURU kwenye wilaya ambazo hazina majengo hayo ikiwemo Wilaya ya Kyerwa kama Mheshimiwa Mbunge anavyoomba.

Mheshimiwa NaibU Spika, Serikali ina nia ya kujenga ofisi kwenye wilaya zote kadri bajeti itakavyoruhusu ili kupunguza gharama za kupanga kusogeza huduma kwa wananchi na kuwafanya watumishi wafanye kazi kwa morali zaidi.

Na. 107

## Ujenzi wa Miradi Mitatu ya Umwagiliaji Malinyi

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA** aliuliza:-

Katika jitihada za kuwezesha Mkoa wa Morogoro kuwa ghala la chakula la Taifa mwaka 2017, Serikali iliahidi kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ujenzi wa skimu tatu za umwagiliaji katika Vijiji vya Usangule, Igawa, Lupunga na Kilosa kwa Mpepo ambazo zitatumia Mito ya Lwasesa, Furuwa na Mwatisi katika Wilaya ya Malinyi:-

(a) Je, ni lini kazi hiyo ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina itakamilika?

(b) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kurekebisha kasoro zilizojitokeza katika mifereji ya skimu iliyojengwa Itete?

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mbunge wa Jimbo la Malinyi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji katika Wilaya ya Malinyi, Serikali katika mwaka 2020/2021 imekusudia kutenga fedha ili kukamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa Skimu ya Kilosa kwa Mpepo ili kupata gharama halisi za ujenzi wa skimu hiyo. Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa skimu zilizosalia za Usangule, Igawa, Lupunga na Utengule ili kujua gharama halisi ya kuendeleza skimu hizo. Aidha, Serikali ipo katika hatua za mwisho za uzinduzi wa Mfuko wa Umwagiliaji kwa lengo la kupata fedha zaidi za usanifu na uendelezaji wa skimu za umwagiliaji ikiwemo skimu ya Itete na zingine katika Wilaya ya Malinyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mikataba ya ujenzi wa skimu za umwagiliaji, mkandarasi hupewa kipindi cha matazamio *(Defects Liability Period)* kwa ajili ya kurekebisha kasoro zitakazojitokeza baada ya kukamilisha ujenzi/ukarabati wa mradi wa umwagiliaji. Kutokana na mvua kubwa iliyonyesha katika msimu wa 2018/2019 na wakulima kushindwa kusimamia ipasavyo miundombinu ya umwagiliaji *(improper management of irrigation infrastructure)* kulijitokeza kasoro katika miundombinu ya Skimu ya Itete. Aidha, kasoro hizo zilisababisha kupungua kwa ufanisi wa ugawaji maji pamoja na maji kubadili mkondo na hivyo kuwepo kwa upotevu wa maji ya umwagiliaji katika skimu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Februari 2019 mkandarasi alifanya marekebisho yote kwa mujibu wa mkataba. Aidha, kwa changamoto za wakulima kuhusu uendeshaji na usimamizi wa miundombinu, Serikali itaendelea kutoa mafunzo ya uendeshaji na utunzaji bora wa miundombinu ya umwagiliaji kwa wakulima ili kuhakikisha miundombinu inakuwa endelevu na pamoja na kujenga uelewa kwa wakulima kuhusu umuhimu wa kuchangia gharama za uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji.

Na. 108

**Umuhimu wa Teknolojia ya Kuhifadhi Mazao**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza:-

Mazao mengi ya wakulima wa viazi, mbogamboga na matunda yanakabiliwa na changamoto ya kuharibika pindi wanapovuna kutokana na kukosekana mbinu za kisasa za uhifadhi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kushirikiana na wadau kueneza teknolojia ya uhifadhi wa mazao ili yaweze kukaa kwa muda mrefu baada ya kuvunwa?

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shally Joseph Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeandaa mkakati wa usimamizi wa mazao baada ya kuvuna. Lengo la mkakati huu ni kuainisha changamoto zilizopo katika mnyororo wa thamani wa mazao kuanzia mazao yanapokomaa hadi yanapomfikia mlaji na mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo. Aidha, mkakati pia umeainisha wadau mbalimbali watakaohusika katika utekelezaji wa mkakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la hifadhi ya mazao, teknolojia mbalimbali zimeainishwa kulingana na aina ya zao kama vile vihenge vya chuma *(metal silo)* na mifuko isiyopitisha hewa ambayo imekuwa ikisambazwa kwa wakulima wa mazao ya nafaka kwa kushirikiana na wadau ikiwemo Kampuni ya *A-Z*, Kampuni ya *IPTL* na Taasisi ya *HELVETAS*. Aidha, teknolojia hizo zimesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza upotevu wa nafaka, kutunza ubora wa mazao na kupunguza matumizi ya viuatilifu ambavyo si salama kwa afya ya mlaji kama vitatumika bila kuzingatia matumizi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hifadhi ya mboga na matunda bado kuna changamoto nyingi kwa kuwa hifadhi ya mazao ya aina hii inahitaji miundombinu makini ya utunzaji na uhifadhi ambayo ina gharama kubwa za kununua na kiutendashaji. Hata hivyo, katika ngazi ya kaya teknolojia ya ukaushaji kwa kutumia mionzi ya jua imekuwa ikisambazwa kwa wakulima ambapo mboga na matunda mbalimbali hukaushwa na kufungashwa vizuri kwa ajili ya matumizi ya baadaye. Aidha. Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine *(SUA)* kinaendelea kuboresha teknolojia rahisi za kuhifadhi mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha wawekezaji katika maeneo ya usindikaji wa mazao ya kilimo ili kuyaongezea thamani kwa lengo la kukabiliana na upotevu wa mazao baada ya mavuno. Serikali imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo

ikiwemo *Save the Children* katika kuandaa miongozo ya mazao ya nyanya, kabichi, bamia, hoho, karoti, matunda na mbogamboga. Aidha, Wizara pia imeendelea kutoa mafunzo ya teknolojia za utayarishaji, uhifadhi na usindikaji wa mazao ya mboga na matunda kwa kutumia majokofu yanayotumia teknolojia ya mkaa na maji vijijini.

Na. 109

**Miradi ya Maji Iliyojengwa chini ya Mpango wa WSDP – Karatu**

**MHE. QUAMBALO W. QULWI** aliuliza:-

Miradi ya Maji katika Vijiji vya Getamock, Kansay, Buger, Endonyawet na Matala iliyojenga chini ya mpango wa *WSDP* haifanyi kazi kutokana na kujengwa chini ya kiwango:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kufufua miradi hiyo ili wananchi wapate huduma ya maji safi na salama?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Qumbalo Willy Qulwi, Mbunge wa Jimbo la Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha miradi iliyojengwa inatoa huduma iliyotarajiwa, Serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini *(RUWASA)* imefanya ukarabati wa Mradi wa Matala kwenye maeneo yote ya mtandao wa bomba yaliyokuwa yanavuja kwa kutumia fedha za malipo kwa matokeo *(Payment by Results)* na huduma ya maji ilianza kutolewa mwezi Julai, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali inatarajia kufanya ukarabati wa Miradi ya Maji ya Getamock na Endonyawet kwenye maeneo yote yaliyobainika kuwa na upungufu ambapo kiasi cha shilingi 112,671.38 kitatumika

kupitia fedha za Malipo kwa Matokeo. Ukarabati wa miradi hiyo umepangwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2020 na mara baada ya kukamilika mradi utaanza kutoa huduma ya maji kwa wananchi. Aidha, mapitio ya usanifu wa miradi ya Kansay na Buger yamekamilika hususan kwenye maeneo yaliyokuwa na upungufu ya kiusanifu kwenye usanifu wa awali. Kiasi cha shilingi 225,000,000.00 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa miradi hiyo utakaohusisha ukarabati wa mtandao wa bomba.

Na.110

## Hitaji la Bwawa Lingine la Maji – Morogoro

**MHE. DEVOTHA M. MINJA** aliuliza:-

Bwawa la Maji la Mindu katika Manispaa ya Morogoro limejaa tope na maji hayatoshelezi wananchi wa Manispaa ya Morogoro:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga bwawa lingine?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimwa Devotha Mathew Minja, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa maji katika Manispaa ya Morogoro na kuhakikisha kiwango cha uzalishaji wa maji kinafikia mahitaji kwa asilimia 100, Wizara ya Maji kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro itatekeleza mradi mkubwa wa maji kutoka chanzo cha Mto Divue ulipo Turiani katika mwaka wa fedha 2020/2021 kwa kutumia fedha za ndani. Mradi huu utakapokamilika unakadiriwa kuongeza uzalishaji maji kwa mita za ujazo 27,000 kwa siku na hivyo kufanya jumla ya uzalishaji wa maji katika

Manispaa ya Morogoro kuwa mita za ujazo 74,000 kwa siku ikilinganishwa na mahitaji ya sasa ya mita za ujazo 67,086.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka 2020/2021, Serikali itapanua mtambo wa kutibu maji wa Mafiga unaotumia chanzo cha Bwawa la Mindu ili uweze kuzalisha mita za ujazo 40,000 kwa siku. Mradi huu utatekelezwa kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo, Ufaransa *(AFD).*

Na. 111

**Kubadili Mfumo wa Elimu Tanzania**

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI** aliuliza: -

Mfumo wa Elimu ya Tanzania unamuandaa zaidi kijana kuajiriwa kuliko kujiajiri na hii ni kutokana na shule kufundisha nadharia zaidi kuliko vitendo:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa upo umuhimu wa kubadili mfumo huo ili ulenge kuajiri vijana wengi zaidi kuliko kutegemea ajira za Serikali?

(b) Je Serikali ina mikakati gani ya kuongeza vyuo vya *VETA*, Kilimo na Mifugo ili vijana wengi zaidi waweze kupata ajira?

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa elimu kwa vitendo kwa ajili ya kumuandaa kijana kuwa na ujuzi unaohitajika katika Soko la Ajira. Kwa kuzingatia umuhimu huo Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuimarisha mafunzo kwa vitendo katika ngazi mbalimbali za elimu. Katika elimumsingi na sekondari, Serikali imehuisha mitaala kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa

stadi mbalimbali za maisha ikiwemo kujumuisha somo la stadi za kazi na ujasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ngazi ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, mitaala inazingatia Soko la Ajira na Umahiri wa Stadi husika *(Competence Based Education and Training-CBET).* Lengo ni kuimarisha mafunzo kwa vitendo ambapo 65% ya mafunzo hufanyika kwa vitendo na 35% nadharia ili kuwawezesha Wahitimu kuajiriwa na kujiajiri. Aidha, Serikali imeunda Mabaraza ya Ujuzi ya Kisekta *(Sectoral Skills Councils)* ambayo yatakuwa kiungo kati ya vyuo vya elimu ya ufundi na wadau kwa lengo la kupata mrejesho kuhusu uwezo wa wahitimu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikakati ya kuongeza Vyuo vya *VETA*, Kilimo na Mifugo, Serikali imeendelea na mikakati ya kujenga na kukarabati vyuo mbalimbali kulingana na mahitaji katika kila Sekta ikiwemo Kilimo na Mifugo. Mfano, katika Sekta ya Elimu, Serikali ya Awamu ya Tano inaendelea na ujenzi wa vyuo 46 vya *VETA* na imekamilisha ujenzi wa vyuo 10 kati ya hivyo. Hivyo, Serikali itaendelea na ujenzi wa vyuo katika sekta mbalimbali kulingana na mahitaji na upatikanaji wa fedha.

Na. 112

## Mikopo isiyo na Riba ya Elimu ya Juu kwa Wanafunzi Wenye Ulemavu

**MHE. AMINA S. MOLLEL** aliuliza:-

Watu Wenye Ulemavu (WWU) ni miongoni mwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu na katika kusoma kwao kuna gharama za ziada za vifaa saidizi hivyo kuwa na mzigo mkubwa wa marejesho tofauti watu wasio na ulemavu:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka kuwapatia watu wenye ulemavu mkopo wa elimu ya juu usio na riba?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapatia ruzuku ya nyezo za kujimudu badala ya mkopo ili kuwaepushia gharama kubwa ya elimu kutokana na ulemavu wao?

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele vya (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikopo ya Elimu ya Juu inayotolewa na Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inaongozwa na Sheria ya Bodi ya Mikopo, Sura 178 ambayo inabainisha kuwa mikopo hiyo ni kwa ajili ya wanafunzi wahitaji *(needy)* wenye sifa za kujiunga na Taasisi za Elimu ya Juu *(eligible).* Lengo la matakwa haya ya kisheria ni kuwawezesha wanafunzi wote wahitaji wanaotoka kwenye familia zenye uwezo mdogo wa kiuchumi kupata elimu ya juu. Aidha, wanafunzi wote wenye ulemavu walioomba na wenye sifa hupatiwa mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikopo ya Elimu ya Juu inayotolewa na Serikali haitozwi riba *(interest)* kama ilivyo kwa mikopo inayotozwa na taasisi za fedha za kibiashara ambayo ni kati ya asilimia 14 hadi 22. Mikopo ya elimu ya juu ya Serikali hutozwa asimilia sita kama Tozo ya Kutunza Thamani *(Value Retention Fee)* ili kutunza thamani ya fedha za mkopo bila kuilazimu Serikali kuongeza fedha za ziada kutunza thamani ya mkopo wa mnufaika. Tozo hii hukatwa kwenye salio la deni *(Outstanding Loan Balance)* na sio kwenye deni la msingi *(Principal Loan).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwawezesha wanafunzi wenye ulemavu kupata elimu ya juu kwa ufanisi, Serikali inapeleka fedha za ruzuku kwenye vyuo vikuu kwa ajili ya kununulia vifaa mbalimbali saidizi vya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Kwa mfano, mwaka 2018/2019, Serikali ilitoa ruzuku ya shilingi 200,000,000.00 ambazo zilipelekwa Vyuo Vikuu vinne vya *UDSM, UDOM, MUCE* na *MoCU* na mwaka 2019/2020 imetenga Sh.250,000,000.00. Aidha Serikali inatoa

ruzuku kwenye vyuo vikuu kwa awamu kulingana na upatikanaji fedha.

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tuna taarifa ya Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijaleta taarifa ya Mheshimiwa Spika kwenu kuna jambo moja ambalo linaleta pia changamoto katika haya ambayo tunayapitia sasa. Wako Waheshimiwa Wabunge ambao wanapeana vile vishkwambi (*tablets*), sasa Mheshimiwa Mbunge anaweza hayupo lakini *tablets* amemwachia Mbunge mwingine na kwa hivyo Mbunge huyo anapiga yeye kura na pia anaonesha kwamba Mbunge huyo mwingine yupo. Sasa inaleta changamoto kidogo hasa kiofisi kwa sababu Mbunge anaweza kuwa hayupo na amepata changamoto huko aliko lakini taarifa za Bunge zinaonesha kwamba yupo kumbe amemwachia mbunge *tablet* yake na kwa hivyo huyo Mbunge anakuja nayo hapa na taarifa za Bunge zinaonekana Mbunge huyo yupo maeneo haya.

Kwa hiyo sasa kwa hili tunalolipita Waheshimiwa Wabunge kila mtu achukue kama ni jukumu lake kuhakikisha anaonesha uongozi katika zoezi hili zima. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wabunge mnatahadharishwa kutokubeba *tablet* ya mtu mwingine na kuonesha kwamba yupo wakati hayupo. Kwa sababu mazingira kama hayo itakuwa ni rahisi tu kufahamu kwamba ni nani alikuwa nayo ya nani na sasa huyo mbunge amepata shida huko aliko lakini takwimu huku Bungeni zinaonesha kwamba alikuwepo ama taarifa zinaonesha taarifa alikuwepo wakati hayupo.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, nilete kwenu taarifa ya kwanza ya Mheshimiwa Spika na taarifa ya kwanza inatolewa kwa mujibu Kanuni ya 33(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Waheshimiwa Wabunge kama mnavyofahamu kwa muda sasa tumekuwa tukichukua jitihada mbalimbali za kujiwekea tahadhari dhidi ya maambuziki ya ugonjwa wa *Corona (COVID 19)* hapa Bungeni. Pamoja na jitihada hizi tumepata taarifa kuwa mmoja wetu tayari amepata maambukizi. Hata hivyo Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika anapenda kuwataarifa kwamba mgonjwa huyo anaendelea vizuri na Serikali inaendelea kumwangalia na kumpatia matibabu stahiki.

Kwa maelezo ya Mbunge huyo ni kwamba alisafiri kwenda Dar es Salaam siku za karibuni na aliporejea, kuanzia Jumatano wiki iliyopita alianza kujisikia dalili kama zilivyotangazwa na wataalam wetu kuhusu virusi hivi vya *corona* na baadaye ikathibitishwa kwamba amepata maambukizi ya virusi vya *corona*.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika anataka kuchukua fursa hii kuwakumbusha na kuwasisitiza tuendelee kuchukua tahadhari za kujikinga na maambukizi ya *corona* kwa kufuata maelekezo ambayo tumekuwa tukipeana mara kwa mara.

Pamoja na maelekezo haya humu Bungeni tumekuwa tukisisitizana kila wakati kwamba mbunge anayeingia Bungeni ambaye ni zamu yake kuingia akae sehemu yake, asikae sehemu ya Mbunge mwingine. Akikaa sehemu ya Mbunge mwingine tukianza kufuatilia nani alikaa karibu na nani, huyu Mbunge anayezunguka humu Bungeni na kukaa kwenye viti vya wengine atatupa wakati mgumu. Kila mtu aone hili linamhusu yeye kama sehemu ya jamii lakini pia kama kiongozi anayetamani yeye kujilinda na kulinda watu wengine.

Kwa hiyo tujitahidi Waheshimiwa Wabunge sana kukaa sehemu zetu ili usitoe virusi sehemu moja ukapeleka sehemu nyingine, lakini pia iwe rahisi kufuatilia kwa uongozi kwamba huyu alikuwa anakaa hapa na changamoto imetokea hapa, tunaweza kuwafuatilia hawa. Sasa ukiwa unazunguka kila sehemu na unakaa kila sehemu na unatumia

kisemeo chochote unakuwa unatuweka sisi sote katika mazingira hatarishi na hata hizi hatua tunazozichukua itakuwa inatuwia ngumu sana kuendelea na huo utaratibu.

Waheshimiwa Wabunge, mara baada ya kikao hiki cha leo kuahirishwa mnatangaziwa kwamba Wabunge wote mtatakiwa kuondoka kabisa maeneo ya Bunge ili kutoa nafasi kwa ofisi na Wataalam wa Wizara ya Afya kuendelea na zoezi la kunyunyiza dawa za kutakasa eneo la Bunge. Kwa hivyo, baada ya kuahirisha shughuli hizi za Bunge Waheshimiwa Wabunge wote kila mtu atatakiwa kuelekea nyumbani kama mlivyoshauriwa na Mheshimiwa Spika, watu mtoke Bungeni–nyumbani – Bungeni. Kwa hiyo bunge hili tutakapoahirisha wabunge mnatarajiwa kuelekea majumbani kwenu wakati hapa Bungeni tutafanya hilo zoezi la kutakasa eneo *(decontamination).*

Waheshimiwa Wabunge ninayo taarifa nyingine ya kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia hiyo hiyo Kanuni ya 33(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2016. Waheshimiwa Wabunge kwa masikitiko makubwa Mheshimiwa Spika anapenda kuwajulisha kuwa Bunge letu limepatwa na msiba mkubwa wa kuondokewa na Mbunge wa Viti Maalum kupitia Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare. Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatere amefariki alfajiri ya leo tarehe 20 Aprili, 2020 katika Hospitali ya Rabininsia Jijini Dar es Salaam alikokuwa amepelekwa kwa ajili ya kupatiwa matibabu.

Waheshimiwa Wabunge kufuatia msiba huo taratibu mbalimbali zimeendelea kufanyika kati ya Ofisi ya Bunge pamoja na familia ya marehemu. Mara baada ya taratibu zote kukamilika tutajulishwa kuhusu ushiriki wetu katika mazishi. Hivyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 152 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kwa siku ya leo hatutaendelea na Kikao cha Bunge badala yake tutakuwa na maombolezo ya msiba wa mwenzetu hadi kesho tarehe 21 Aprili, 2020. Waheshimiwa Wabunge naomba sasa tusimame kwa muda

wa dakika moja kama ishara ya kumkumbuka na kuomboleza kifo hiki cha mwenzetu.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walisimama kwa dakika moja kuomboleza kifo cha Mheshimiwa Mch. Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare)*

**NAIBU SPIKA:** Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya taarifa hizi za Mheshimiwa Spika naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya kesho tarehe 21 Aprili, 2020, saa nane kamili mchana.

*(Saa 8.34 Mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne Tarehe 21 Aprili, 2020 Saa Nane Mchana)*